**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**FASIHI**

**MUDA: SAA 2 ½**

## JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KIDATO CHA NNE 2018

### Maagizo

a) Jibu maswali manne pekee
b) Swali la kwanza ni la lazima.
c) Maswali mengine matatu ya chaguliwe kutoka sehemu zilizobaki yaani; Riwaya, Tamthilia,Fasihi Simulizi na Hadithi Fupi.
d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
e) Kila swali lina alama ishirini(20)
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
g) Karatasi hii ina kurasa 3 zilizopigwa chapa.
h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

1. Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na wa ng'ambo,
   Kwani ngoja 'mesikia, inaumiza matumbo,
   Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimo mbo,
   Yafaa jihadharia, maisha yas,ende kambo;

2. Maisha yas'ende kombo, kututoa yetu ari,
   Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,
   Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
   Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari

3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahana,
   Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
   Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatuuma.
   Watoto tunayo mori, mi lini mtajakoma?

4. Ni nani mtajakoma, na pombe ziso halali?
   Sio baba sio mama, mbona ny'hamtujali
   Mwafa ja nzi twasema, mwatuacha bila hali
   Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila mwapigana
   Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona
   Mwatusumbua akili, twaumia tena sana
   Achene na ukatili, kwani upendo hamna,

6. Kwani upendo hamna, Kama mbwa mwatuchapa
   Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa
   Pa kujificha hatuna, tumebaki tukitapa
   Maisha hamu hayana, timevunjwa na mifupa.

7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,
   Mwatubaka na kuapa, kutung'ata nyi' majitu,
   Maisha hatujakopa, fahamu mkosa utu,
   Hayo makeke na pupa, mtakoma utukutu,

8. Mtakoma utukutu, na kutumia mikiki,
   Na tabia zenye kutu, tumechoka nay chuki,
   Hatutakubali katu, kutendewa yenya siki,
   Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki.

Maswali

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
b) Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
c) Taja nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)
d) Eleza bahari nne zinazowakilishwa katika shairi hili. (alama 4)
e) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
f) Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)

g) Huku ukitoa mfano taja mfano mmoja wa uhuru wa mshairi ambao umetumiwa katika shairi hili. (alama 2)

**<u>SEHEMU YA B:</u>**
**<u>RIWAYA KIDAGAA KIMEMWOZEA K. WALIBORA</u>**

**<u>Jibu swali la 2 au la 3</u>**

2. "Dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika alaa kulihali"

    a) Eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika.
    b) Thibitisha ukweli kuwa dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika kwa kumulika matukio riwayani. (alama 12)

3. Uchochole umekithiri katika jamii anayotuchorea mwandishi. Thibitisha kauli hii kisha utambue chanzo chake. (Alama 20)

**<u>SEHEMU YA C: TAMTHILIA KIGOGO PAULINE KEA</u>**
**<u>Jibu swali la 4 au la 5</u>**

4. "Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka……"

    a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
    b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapinduzi? (alama 8)
    c) Taja sifa zozote nane za muhusika huyu (alama 8)

5. Tamthilia ya 'Kigogo' ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha. (alama 20)

**<u>SEHEMU YA D: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINEZO</u>**
**<u>Jibu swali la 6 au la 7</u>**

**6. "Rasta twambie bwana!"**

    a) Weka dondo katika muktadha (ala 4)
    b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (ala 2)
    c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe? (alama 4)
    d) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu ya hadithi hii. (alama10 )

7. Jadili mashaka ya Mashaka katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka" (alama 20)

**<u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMJULIZI</u>**

**<u>8.</u>**

a) Fafanua mambo yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (alama 10)
b) Eleza maana ya lakabu. (alama 2)
c) Sifa za lakabu ni zipi? (alama 4)
d) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii. (alama 4)